**Halmashauri ya Songea ilivyodhamiria kupima viwanja mji mzima wa kihistoria wa Peramiho**

**Mji** wa Peramiho uliopo Wilaya ya Songea Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa miji ya zamani yenye historia ya kipekee katika ukanda ya kusini.



Mji huo unafahamika zaidi nje ya nchi pengine kuliko miji mingine iliyopo kusini mwa Tanzania kutokana na mji huo kuwa na historia ya namna yake kipekee ikiunganisha Tanzania na mataifa ya Ulaya.

Historia ya mji wa Peramiho uliopo kilometa 24 tu kutoka makao makuu ya mkoa wa Ruvuma Songea inaunganishwa na wabenediktini wa kanisa katoliki kutoka St.Otilia nchini Ujerumani,ambao waliamua kuweka makao makuu yao katika Abasia ya Peramiho.

Wabeneditine hao waliingia kwa mara ya kwanza katika mji huo mkongwe mwaka 1898 wakiongozwa na Kasian Spiss.Tangu wakati huo wabenediktine hao wamekuwa wakifanya mambo yanayoutangaza mji huo hali iliyosababisha kuutambua mji wa Peramiho kuwa ni mji unaokidhi vigezo kuwa mji wenye utalii wa kiutamaduni.

Kutokana na umuhimu wa Mji mdogo wa Peramiho,Halmashauri ya Wilaya ya Songea kupitia Idara ya Mipango mji kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la Aga Teo Hope Foundation wanatekeleza mradi wa urasimishaji wa viwanja 5260 katika mji mzima wa Peramiho.

Afisa Mipango Miji wa Halmashauri hiyo Meliladius Aliefao anasema zoezi hilo limelenga kurasimisha mji mzima wa Peramiho ambapo anasema Taasisi ya Aga Teo Hope Foundation imeletwa kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhakikisha kila kipande cha ardhi katika mji wa Peramiho na Halmashauri ya Wilaya hiyo vinapimwa.



"Mkoa wa Ruvuma umewekewa lengo la kurasimisha kwa mwaka watu 7000,sisi kama Halmashauri tumejiwekea ndani ya miezi mitatu kutoka sasa kurasimisha viwanja wananchi zaidi ya 5000",anasema Aliefao.

Anasema hadi kufikia Desemba mwaka huu watu zaidi ya 5000 watakuwa wamerasimishwa viwanja vyao kwa kupimiwa, kupangiwa na kumilikishwa na kwamba katika zoezi hilo wananchi wanachangia gharama kulingana na mkubaliano baina ya Halmashauri,Taasisi ya AgaTeo na wananchi wenyewe.

Afisa Mipango Miji huyo anasema wananchi wamekubali kuchangia kiasi cha shilingi 150,000 ambayo hawatalazimika kuichangia kwa mara moja kwa sababu Taasisi ya Aga Teo imefadhili sehemu kubwa ya gharama zinazohitajika kutekeleza mradi huo.

Anasema hadi sasa tayari wananchi wameunda Kamati zao na kufungua akaunti zao ambazo wataweka michango yao taratibu na kwamba wananchi watalazimika kukamilisha michango yao hadi hapo Halmashauri itakapokamilisha hati zao.

"Zoezi hili la urasimishaji kwa kuanzia linafanyika katika kata sita za Halmashauri ya Wilaya ya Songea,tumeanza na mji wa Peramiho zoezi linakwenda kwa kasi,tuna vifaa vya kisasa,baada ya miezi mitatu tutakuwa tumemilikisha mji mzima wa Peramiho",anasisitiza Aliefao.

Anatoa rai kwa Halmashauri nyingine nchini kuiga mfano wa Halmashauri hiyo ili kutatua migogoro ya ardhi,kupata mapato ya serikali na wananchi kuwa na ardhi yenye thamani hali ambayo itachangia kuleta maendeleo kwa wananchi.

Kwa upande wake William Mapunda ambaye ni Mratibu wa Taasisi ya Aga Teo Hope Foundation anasema wanatekeleza mradi wa urasimishaji wa viwanja katika Halmashauri ya Songea na kwamba Taasisi hiyo ilisajiriwa kwa mujibu wa sheria mwaka 2019 kupitia TAMISEMI na kazi kubwa ya Taasisi hiyo ni kurasimisha ardhi na mashamba katika miji na vijiji.

Mapunda anasisitiza kuwa wamedhamiria kuhakikisha kuwa wananchi wanapata hatimilki ambazo zitawezesha kukopesheka na Taasisi za kifedha kwa upande wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea na mbegu.

Anazitaja kata sita ambazo wanaanza kutekeleza mradi wa urasimishaji ardhi kuwa ni Kata ya Peramiho,Liganga, Kilagano, Litisha,Parangu na Mbingamhalule.

Anasema mradi huo unatarajia kukamilika baada ya miezi sita na kwamba kazi ya usajiri inaendelea katika kata ya Peramiho ambapo hadi sasa watu zaidi ya 600 wamejisajiri kwa ajili ya uhakiki wa viwanja na kujaza fomu ili kupata hatimiliki.



Mapunda anasema ili kuhakikisha kazi ya urasimishaji inakwenda ndani ya muda,Kamishina wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma ametoa mashine maalum inayotumia satellite yenye uwezo wa kupima umbali wa kilometa 30 sanjari na wafanyakazi watano wakiwemo wataalam wa mipango miji.

“Tunaishukuru Ofisi ya Kamishina wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma kwa kutupatia mtambo wa kisasa wa kupima ardhi ambao unatuwezesha kufanyakazi kubwa

kwa muda mfupi,kwa namna ya pekee tunamshukuru Rais Magufuli kwa kutambua umhimu wa urasimishaji katika nchi nzima”,anasema Mapunda.

Hata hivyo Mapunda anasema ili kutekeleza kwa vitendo zoezi aliloagiza Waziri wa Ardhi William Lukuvu,Taasisi yake imedhamiria kuhakikisha kila kipande cha ardhi na mashamba wilayani Songea vinapimwa ili wananchi na serikali iweze kukusanya maduhuli yake na kuweze kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Anasema mara baada ya kupima viwanja vyote katika mji wa Peramiho sasa mji huo utaondoka kutoka katika hali ya vijiji na kuwa mji rasmi.

Kwa upande wake Bernad Rwechungura Katibu Mtendaji wa Aga Teo Foundation anasema wananchi wa Mji wa Peramiho wamelipokea zoezi la urasimishaji ardhi kwa shangwe kubwa ambapo idadi kubwa ya wananchi wanafika kujisajiri kwa ajili ya mchakato wa kupata hatimiliki.

Anasema hadi sasa watu zaidi ya 700 wamejisajiri na watu waliorudisha fomu ni zaidi ya 300 ambapo anasema hali hiyo inadhihirisha kuwa watu wamechoka na migogoro ya ardhi hivyo wanapenda kuona ardhi yao inakuwa na hati inayoeleweka.

“Wananchi wengi sasa ni wazalendo wanahitaji hatimiliki ili waweze kulipa kodi za ardhi na majengo serikalini,lengo letu ni kupima kila kipande cha ardhi kulingana na sheria ya ardhi ya mwaka 1999 iliyotokana na sera ya ardhi ya mwaka 1995 ”,anasema Rwechungura.

Hata hivyo Mtaalam huyo wa ardhi anasema Tanzania tayari ilikuwa na malengo yake ya mwaka 2025 ya kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kitapimwa na kwamba hata malengo 17 ya millennia ya Dunia endelevu yanaeleza kuwa kila kipande cha ardhi duniani kitapimwa.

Rwechungura anashauri Tanzania nzima ipimwe na serikali ipate mapato yake kulingana na kodi zitakazokuwa zinalipwa.

Mariana Ponera(80) ni Mkazi wa Mji wa Peramiho akizungumzia urasimishaji unaendelea Peramiho anaishukuru serikali kwa sababu ardhi itakuwa na ulinzi kwa watoto wake.

Sadaka Komba mkazi wa Peramiho anasema urasimishaji wa viwanja na kumilikisha ardhi kutamaliza migogoro ya ardhi ambayo imekuwa inaibuka mara kwa mara katika jamii na kwamba serikali pia itaongeza mapato yanayotokana na kodi ya ardhi.

**Makala hii imeandikwa na Albano Midelo**

**Afisa Habari Mkoa wa Ruvuma**

**Mawasiliano simu 0784765917**